# Je, niko katika hatari ya kupata Hepatitis B?

**Ni ugonjwa wa aina gani?**

Hepatitis B ni virusi vinavyoenea katika ini na kusababisha madhara makubwa katika ini. Ini ni muhimu mwilini na kazi yake ni kusaga vyakula pamoja na kemikali zinazoleta madhara, kutengeneza protini na kuhifadhi vitamini muhimu, madini, na sukari.

**Je, ugonjwa huu umesambaa?**

Kuna watu kadiri ya milioni 350 duniani, ambao wameambukizwa na ugonjwa huu wa hepatitis B.

Kuna wagonjwa wapya kadiri ya 600 – 800 wanaoishi Uingereza na Wales, na kila mwaka kunakuwa na idadi mpya ya wagonjwa kati ya 50 - 60 nchini Wales. Idadi hii ni ndogo ukilinganisha na nchi zingine ingawa watu wengi wanaweza kuwa na ugonjwa huu bila wao kujua.

**Dalili zake ni zipi?**

Idadi kubwa ya watu wenye hepatitis B hawajijui kama wameambukizwa kwa sababu hawaonyeshi dalili zozote. Watu wengine wanaweza kuwa na dalili kadhaa wanapoambukizwa kwa mara ya kwanza. Wanaweza kuwa na aina fulani ya mafua, kuwa na uchovu sana, kukosa hamu ya kula, ngozi na macho kubadilika rangi ya njano (homa ya manjano); na/au mkojo mweusi. Yoyote mwenye ugonjwa huu anaweza kuambukiza watu wengine, hata kama hana dalili yoyote au hata kama hajui kama anaumwa. Njia pekee ya kujua kama umeambukizwa na Hepatitis B ni kupima damu ili kugundua uambukizo.

**Maelezo zaidi kuhusu hepatitis B**

Idadi kubwa ya wagonjwa watu wazima huwa wanapata nafuu ya ugonjwa huu. Ijapokuwa, kati ya watu 100 wenye ugonjwa huu:

- mtu 1 anaweza kuwa na madhara makali yanayosababisha maini yasifanye kazi vizuri mara baada ya kuambukizwa; na
- watu kama 5 wataendelea kuwa na ugonjwa huu kwa muda mrefu – watakuwa wabebaji wa virusi na wanaweza kuambukiza watu wengine. Angalau mbebaji 1 atapata madhara makali ya ugonjwa wa ini maishani.

Watoto na watoto wachanga walioambukizwa ugonjwa huu wa hepatitis B wana uwezo mkubwa wa kuwa wabebaji wa virusi, ijapokuwa ukiwalinganisha na watu wazima, watoto wana uwezo mdogo wa kuonyesha dalili zozote za ugonjwa. Mara nyingi mtoto mgonjwa anakuwa na virusi hivi mwilini kwa muda mrefu wa maisha yake na kuna uwezo mkubwa wa kuwekeza ugonjwa huu mwilini na kuumwa ini kwa muda mrefu.

Tiba ya hepatitis B bado haijapatikana ingawa kuna matibabu ambayo yanaweza kusaidia ini lisiendelee kuharibika na virusi visiendelee kuzaliana. Mafanikio ya chanjo yanatofautiana kati ya watu tofauti.

Kuna aina zingine za magonjwa ya hepatitis, kama vile hepatitis A na hepatitis C, ambayo ni tofauti na hepatitis B.

**Unapataje ambukizo la ugonjwa huu?**

Hepatitis B ni virusi vilivyopo katika damu na katika majimaji ya miili ya wagonjwa. Ni ugonjwa unaosambaratika kirahisi. Huambukizwa kwa njia ya kujamiiana kati ya mtu mwenye uambukizo na asiyenao kwa njia ya:

- kujamiiana na mtu mwenye uambukizo bila kutumia kondomu (ngono kati ya mwanamke/mwanamme na mwanamme/mwanamme). Hii ni hatari kwa sababu majimaji ya mwili yanaweza kuwa na virusi;
- kutoka kwa mama mgonjwa hadi kwa mtoto wake;
- kuchangia vifaa vya kujitunga madawa ya kulevya (kama vile sindano, vijiko, maji na vichujio);
- kuchangia miswaki, mashine ya kunyolea au vifaa vya kuchorea mwili na vya kutoboa ngozi visivyotakaswa vizuri; au
- kuongezewa damu (kwa mfano kupokea damu iliyoambukizwa na virusi au vifaa vya damu).

**Nani yuko katika hatari ya kuambukizwa?**

Watu walioko katika vikundi vifuatavyo wanaweza kuwa katika hatari ya kuambukizwa na hepatitis B:

- watoto wanaozaliwa na mama mwenye uambukizo;
- mwenza, mtoto, au mtu anayeishi nyumbani mwenye uambukizo;
- watu wanaofanya kazi katika sehemu ambazo wanaweza kushika majimaji ya mwili, kwa mfano madaktari, manesi, daktari wa meno, maafisa wa magereza, au polisi;
- mtu anayefanya mapenzi na watu tofauti mara kwa mara, haswa wale ambao hawatumi kondomu; au
- mtu anayejidunga sindano ya madawa ya kulevya na kuchangia vifaa vya kujidunga madawa.

Kama unafikiri wewe, au mtu yoyote katika familia yako, anaweza kuwa hatarini ni vizuri kumueleza daktari wako, au nesi, au kliniki ya tiba ya magonjwa ya mfumo wa uzazi na mkojo (GUM).

Kama utasafiri na kwenda katika nchi ambayo hepatitis B imesambaratika kuna hatari ya kupata ugonjwa. Unaweza kushauriana na GP, au na nesi wako au na kliniki na kuangalia kama utahitaji kuchanjwa, wao watakupa ushauri mzuri kuhusu chanjo na vitu vya kuepuka wakati unaposafiri nje ya nchi ili usiambukizwe.

**Naweza kujikinga na ugonjwa wa hepatitis B?**

Ndio. Kuna chanjo nzuri sana inayopatikana. Kama unafikiri uko katika hatari kubwa ya kupata hepatitis B ongea na GP, nesi wako, au na kliniki ya tiba ya magonjwa ya mfumo wa uzazi na mkojo. Wao watakusaidia kuamua kama kuna haja ya wewe kuchanjwa ili uwe na kinga na pia wanaweza kukupa ushauri wa kupunguza hatari ya uambukizo.

**Dawa ya chanjo ya Hepatitis B ni nini?**

Hepatitis B ni chanjo ambayo kwa kawaida hutolewa kama dozi ya chanjo 3. Chanjo hii ni salama na nchi nyingi duniani zinaitumia ikiwa ni utaratibu wa kawaida wa kuchanja watoto. Ni jambo la muhimu sana kumaliza dozi yote ili ifanye kazi yake vizuri.
Kama unafikiri uko katika hatari ya kupata hepatitis B ongea na GP au na nesi wako. Au wasiliana na kliniki ya tiba ya magonjwa ya mfumo wa uzazi na mkojo wakupe ushauri wa siri, bila wewe kujulikana na wanaweza kukupima damu.

**Naweza kupata wapi maelezo zaidi?**

Unaweza kuwapigia simu NHS Direct Wales ukitumia namba hii
0845 46 47
au
Tazama tovuti ya Public Health Wales iliyopo hapa:
www.publichealthwales.wales.nhs.uk/

au kutoka:

The British Liver Trust
2 Southampton Road, Ringwood, BH24 1HY
Simu ya Bure: 0800 652 7330
General enquiries: 01425 481320
Fax: 01425 481335
Email: info@britishlivertrust.org.uk
www.britishlivertrust.org.uk
© Crown Copyright 2010 E749